**AFRICAN UNION**

الاتحاد الأفريقي

**UNION AFRICAINE**

**UNIÃO AFRICANA**

**AFRICAN COURT ON HUMAN AND PEOPLES' RIGHTS**
**COUR AFRICAINE DES DROITS DE L'HOMME ET DES PEUPLES**

S.L.P. 6274 Arusha, Tanzania Simu: +255 27 2970 430/431/432
Tovuti www.african-court.org Barua pepe. registrar@african-court.org

AFCHPR/PTS/2023/093
Tarehe: 03 Aprili 2023

# WITO WA KUTANGAZA NIA

# KUANZISHA KANZIDATA YA WATAALAM WA KUJITEGEMEA WALIOKIDHI VIGEZO

## WAFASIRI WA KUJIHARIRI

## I. UTANGULIZI

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilianzishwa chini ya Itifaki ya mwaka 1998 ya Haki za Binadamu na Watu na kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binandamu na Watu (Itifaki). Itifaki hii ilianza kutumika rasmi tarehe 25 Januari 2004, na kuruhusu uanzishwaji wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu (AFCHPR). AFCHPR ni chombo cha kwanza cha kimahakama barani Afrika chenye jukumu la kulinda haki za binadamu na watu. Mamlaka ya msingi ya Mahakama hii ni kutimiza jukumu la Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu iliyopo Banjul la kulinda haki za binadamu na watu. Makao makuu ya Mahakama hii yapo Arusha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## II. NIA NA MADHUMUNI

Ili kuboresha kanzidata yake, Mahakama inatangaza na fasi za kazi kwa wafasiri wahariri wenye sifa zinazostahili ambao ni raia wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika wenye lugha za Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kiswahili kutuma maombi yao.

***Zingatia: Wale ambao wametuma maombi hapo awali na kujulishwa kuwa wamefaulu kujumuishwa kwenye kanzidata hawahitaji kutuma maombi tena.***

## III. WIGO

Wafasiri wahariri wa kujitegemea wanaalikwa kuonesha nia ya kutoa huduma ya ana kwa ana na kwa njia ya mtandao (kwa mfano, wakati wa vikao na mikutano ya Mahakama). Watapewa mikataba kwa ajili ya ufasiri na uhariri wa nyaraka za Mahakama.

## IV. MAJUKUMU

Wafasiri wahariri wa kujitegemea watatoa huduma bora za ufasiri na uhariri wa nyaraka za Mahakama kwa wakati unaotakikana kwa kutumia istilahi stahiki.

## V. VYETI VINAVYOHITAJIKA

- Shahada ya Uzamili katika Tafsiri, Sayansi ya Binadamu na Lugha au nyanja yoyote inayohusiana na fani hizi na uzoefu usiopungua miaka mitano (5) ya ufasiri, ikijumuisha mitatu (3) ya uhariri au ya kujihariri (hasa katika (ma)shirika la kimataifa). Sifa ya juu katika eneo husika itakuwa sifa ya ziada.
- Au Shahada ya Kwanza katika Tafsiri, Sayansi ya Binadamu na Lugha au nyanja yoyote inayohusiana na fani hizi na uzoefu usio pungua miaka saba (7) ya ufasiri, ikijumuisha mitatu (3) ya uhariri au ya kujihariri (hasa katika shirika la kimataifa).
- Uzoefu katika kazi ya Mahakama hii na mahakama nyingine za kimataifa na / au za kitaifa utakuwa sifa ya ziada.
- Msingi wa sheria au umahiri wa istilahi za kisheria utakuwa sifa ya ziada.

## VI. UJUZI UNAOHITAJIKA

- Ujuzi wa tarakilishi (kutumia vema zana za MS Office: Word, Excel, PowerPoint, PDF, n.k.)
- Uwezo wa kuunda nyaraka.
- Maarifa ya zana za tafsiri zinazosaidiwa na tarakilishi (CAT) (kwa mfano, Trados) itakuwa sifa ya ziada.
- Uwezo wa kufanya kazi ana kwa ana au kwa njia ya mtandao ndani ya muda mfupi na chini ya usimamizi mdogo.

## VII. MALIPO

- Tafsiri na marekebisho ya mtandaoni:
  *US$ 125/1,000 maneno;*
  *US$130/1000 maneno kwa hati za dharura.*
- Tafsiri na masahihisho ya ndani (vikao na mikutano mingine)

*US$ 300 kwa siku + pesa za kujikimu kila siku* kulingana na mahali zinapofanyika shughuli za Mahakama.
Mahakama itagharamia safari kwa wale wenye mikataba ya shughuli za ana kwa ana kwa kuzingatia sera za Umoja wa Afrika zinazohusu safari (Tiketi moja ya ndege kwenda na kurudi ya daraja la kiuchumi).
Malipo yote yatafanywa kwa kufuata sheria na taratibu za Umoja wa Afrika.
Mahakama inayo haki ya kubadilisha viwango tajwa hapo juu wakati wowote.

## VIII. VIGEZO VYA TATHMINI

- Sifa za kitaaluma (alama 30)
- Uzoefu wa kitaaluma (alama 40)
- Ustadi wa kompyuta (alama 10)
- Umahiri wa zana za kutafsiri (k.m., Trados) (alama 15)
- Mchanganyiko wa lugha (alama 5)

## IX. MASUALA YA KUZINGATIA KATIKA MAOMBI

Maombi yanapaswa kujumuisha:

- Fomu ya mwombaji iliyojazwa (imeambatishwa), ikisema (mi)mchepuo wa lugha (kwa mfano, EN / AR: EN / FR; EN/PT; EN/SW, n.k.)[1]
- Nakala za vyeti, uthibitisho, n.k.
- Nyaraka za ziada na maelezo ya kina juu ya uzoefu wa kazi (mikataba, viwambo vya barua pepe zinazohusiana na mikataba ya tafsiri (moja kwa kila mwaka wa uzoefu), n.k).

***Zingatia: Maombi yanayoonesha sifa za kitaaluma na uzoefu wa kazi usioendana na nakala za vyeti, mikataba na / au viwambo au agizo la ununuzi wa mikataba hiyo haitazingatiwa.***

## X. UWASILISHAJI WA MAOMBI

Maombi lazima yataje katika kichwa cha habari **"TANGAZO LA MAOMBI YA KUINGIA KWENYE KANZIDATA YA WAFASIRI WA KUJIHARIRI WA KUJITEGEMEA WA MAHAKAMA YA AFRIKA".**

*Maombi yanapaswa kutumwa kwa barua pepe kupitia: tender@african-court.org*
(*Ukubwa wa juu wa viambatisho ni MB 25. Ikiwa ukubwa wa viambatisho unazidi MB 25, tafadhali tuma kwenye barua pepe tofauti).*
*Kwa sababu za usalama, Viungo vya URL vya kupakua viambatisho kutoka kwa vyanzo vya "Clouds" havitafunguliwa. Nyaraka zinapaswa kuambatanishwa na barua pepe.*

[1] Kiingereza/Kiarabu; Kiingereza/Kifaransa; Kiingereza/Kireno; Kiingereza/Kiswahili, n.k.

Au
Kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:
***Msajili wa Mahakama,***
***Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu***
***S.L.P 6274***
***Arusha, Tanzania***
Au
Kuwasilisha moja kwa moja Idara ya usajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, TANAPA, Mwalimu Julius Nyerere Conservatory Centre, Phase II, Dodoma Road. Arusha, Tanzania.

## XI. TAREHE YA MWISHO YA KUWASILISHA MAOMBI

**Mwisho wa kupokea maombi ni saa 11:00 jioni (GMT+3) tarehe 03 mei 2023.**
Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na sisi kupitia barua pepe ifuatayo: procurement@african-court.org

***Zingatia: Maombi yatakayo pokelewa baada ya tarehe ya mwisho na/au kupitia anwani tofauti na zile zilizotajwa chini ya kifungu "X. UWASILISHAJI WA MAOMBI", na/au kutoambatanishwa na nakala za vyeti za kitaaluma na ushahidi wa uzoefu wa kitaaluma, na/au bila Fomu ya Ushauri iliyojazwa na kusainiwa itakataliwa.***

**Dkt. Robert W. Eno**

**Msajili wa Mahakama**